



RESEARCH ARTICLE

Sauti za Ziواني: Uchambuzi wa Nyimbo za Uvuvi za Kisukuma kama Chombo cha Mawasiliano ya Jamii katika Mwambao wa Ziwa Victoria

Steven Yesaya

Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Tanzania

Corresponding Author

Steven Yesaya, Email: steveyesaya1@saut.ac.tz

Author's Contributions

All authors contributed equally to this research.

Article History

Received February 9, 2026; Accepted: April 13, 2026; Published: July 24, 2026.

IKISIRI

Makala hii inachunguza mchango wa nyimbo za uvuvi za Kisukuma kama chombo cha mawasiliano ya jamii na maendeleo ya kijamii miongoni mwa wavuvi wa mwambao wa Ziwa Victoria. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Uamilifu iliyoasisiwa na Bronislaw Malinowski, A.R. Radcliffe-Brown na Franz Boas. Data zilikusanywa kupitia usaili na ushuhudaiji shirikishi miongoni mwa wavuvi wa jamii ya Wasukuma katika ziwa Viktoria Mkoa wa Mwanza. Matokeo yanaonesha kuwa nyimbo za uvuvi hutumika kuhamasisha uwajibikaji, kuimarisha mshikamano, kueleza hisia mbalimbali na kutoa tahadhari kuhusu hatari zinazoweza kujitokeza ziwani. Aidha, nyimbo hizi huchangia katika kuhifadhi maarifa ya jadi na kuendeleza maadili ya kazi. Makala inahitimisha kuwa nyimbo za uvuvi za Kisukuma ni zaidi ya burudani; ni nyenzo muhimu ya mawasiliano na urithi wa kitamaduni unaostahili kuhifadhiwa na kuendelezwa.

Keywords: Nyimbo za uvuvi; Wasukuma; mawasiliano ya jamii; fasihi simulizi; Nadharia ya Uamilifu

UTANGULIZI

Nyimbo ni mojawapo ya tanzu muhimu za fasihi simulizi zinazotumika kuhifadhi na kuwasilisha maarifa, maadili, historia na uzoefu wa jamii husika. Katika jamii nyingi za Kiafrika, nyimbo zimekuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano inayotumiwa kuelimisha, kuonya, kuhamasisha na kuburudisha wanajamii. Kwa mujibu wa M.M. Mulokozi (1996), nyimbo ni utanzu wa ushairi wa fasihi simulizi unaoimbwa na kuambatana na muziki wa sauti, huku ukiwasilisha ujumbe wenye maana kwa jamii. Vivyo hivyo, J.H. Nketia (1963) anabainisha kuwa nyimbo huakisi shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini zinazofanywa na wanajamii katika mazingira yao ya kila siku. Hivyo, nyimbo si chombo cha burudani pekee bali ni nyenzo muhimu ya mawasiliano na ujenzi wa maarifa ya kijamii. Katika shughuli za kiuchumi, nyimbo zimekuwa zikitumika kama nyenzo ya kuratibu kazi, kuhamasisha

uwajibikaji na kuimarisha mshikamano miongoni mwa washiriki wa shughuli husika. Katika mazingira ya uvuvi, nyimbo huwasaidia wavuvi kuwasiliana, kutiana moyo wanapokabiliwa na mazingira magumu ya kazi, kutoa tahadhari kuhusu hatari zinazoweza kujitokeza na kusherehekea mafanikio yanayopatikana kutokana na shughuli za uvuvi. Aidha, nyimbo hizo hubeba maarifa ya jadi kuhusu mazingira ya majini, hali ya hewa na mbinu za uvuvi ambazo hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa sababu hiyo, nyimbo za uvuvi zina nafasi kubwa katika kuendeleza shughuli za uzalishaji mali pamoja na kudumisha mshikamano wa kijamii miongoni mwa wavuvi.

Miongoni mwa jamii zinazotumia nyimbo katika shughuli za uvuvi ni jamii ya Wasukuma wanaoishi katika maeneo mbalimbali yanayozunguka Ziwa Victoria. Wasukuma ni miongoni mwa makabila makubwa nchini Tanzania, wakipatikana katika mikoa

ya Mwanza, Simiyu, Geita, Shinyanga, Mara na baadhi ya maeneo ya Tabora. Mbali na kujishughulisha na kilimo na ufugaji, baadhi ya Wasukuma wanaoishi katika mwambao wa Ziwa Victoria hujihusisha na shughuli za uvuvi kama chanzo muhimu cha chakula na kipato. Kutokana na mazingira hayo, nyimbo za uvuvi zimeendelea kuwa sehemu muhimu ya maisha yao ya kila siku, zikitumika katika kuwasilisha taarifa, kuhamasisha kazi na kujenga mahusiano ya kijamii miongoni mwa wavuvi.

Licha ya kuwepo kwa tafiti mbalimbali zilizojadili nyimbo kama sehemu ya fasihi simulizi na mchango wake katika jamii, bado kuna upungufu wa tafiti zinazochunguza kwa kina nafasi ya nyimbo za uvuvi za Kisukuma kama chombo cha mawasiliano ya jamii. Tafiti nyingi zimejikita katika nyimbo za jadi kwa ujumla bila kuangazia kwa undani namna nyimbo za uvuvi zinavyotumika kuwasilisha taarifa, kujenga mshikamano, kuhamasisha uwajibikaji na kutoa tahadhari katika mazingira ya kazi za uvuvi. Pengo hili la maarifa ndilo lililochochea kufanyika kwa utafiti huu unaolenga kuchunguza mchango wa nyimbo za uvuvi za Kisukuma kama chombo cha mawasiliano ya jamii miongoni mwa wavuvi wa mwambao wa Ziwa Victoria. Kupitia uchunguzi huu, makala inakusudia kuongeza maarifa kuhusu nafasi ya fasihi simulizi katika kuendeleza mawasiliano na shughuli za kiuchumi katika jamii za Kiafrika.

Sababu za Kutumia Nyimbo za Uvuvi za Kisukuma kama Nyenzo za Mawasiliano

Nyimbo za uvuvi za Kisukuma zimeendelea kuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano miongoni mwa wavuvi na wanajamii wanaoishi katika mwambao wa Ziwa Victoria. Tofauti na mawasiliano ya kawaida yanayotegemea mazungumzo ya moja kwa moja, nyimbo hizi hutumia lugha ya kisanaa inayoweza ujumbe kufikishwa kwa urahisi, kuvutia wasikilizaji na kudumu katika kumbukumbu za jamii. Kutokana na mazingira ya kazi ya uvuvi yanayohitaji ushirikiano wa karibu na mawasiliano ya haraka, nyimbo zimekuwa chombo muhimu cha kurahisisha mawasiliano na kuimarisha mshikamano wa kijamii miongoni mwa wavuvi.

Sababu mojawapo ya matumizi ya nyimbo hizi ni uwezo wake wa kuwasilisha taarifa zinazohusu shughuli za uvuvi. Wavuvi hutumia nyimbo kutoa taarifa kuhusu maeneo yenye samaki wengi, mabadiliko ya hali ya hewa, muda wa kuanza au kusitisha shughuli za uvuvi na tahadhari mbalimbali zinazohusiana na usalama ziwani. Kupitia nyimbo hizo, ujumbe unaweza kuwafikia

watu wengi kwa wakati mmoja na kwa namna inayoeleweka kwa urahisi kutokana na uzoefu wa pamoja wa wanajamii husika.

Aidha, nyimbo za uvuvi hutumiwa kuhamasisha ari ya kazi na kuwajengea wavuvi moyo wa kujituma katika shughuli zao. Uvuvi ni kazi inayohusisha changamoto nyingi, ikiwemo uchovu, hatari za mawimbi makubwa, upepo mkali na mazingira magumu ya kazi. Katika mazingira hayo, nyimbo huwapa wavuvi nguvu ya kuendelea na kazi, kuondoa hofu na kuongeza matumaini ya kupata mafanikio. Kwa njia hii, nyimbo zinakuwa chombo cha mawasiliano kinachobeba ujumbe wa motisha na uwajibikaji.

Sababu nyingine ni kwamba nyimbo za uvuvi huimarisha mshikamano na ushirikiano miongoni mwa wavuvi. Wakati wa shughuli za uvuvi, mafanikio hutegemea ushirikiano wa washiriki wote katika kuvuta nyavu, kuendesha vyombo vya uvuvi na kutekeleza majukumu mengine kwa pamoja. Kuimba kwa pamoja huwafanya wavuvi wajisikie kuwa sehemu ya kundi moja na hivyo kuimarisha uelewano, kuaminiana na mshikamano wa kijamii. Hali hii huongeza ufanisi wa kazi na kupunguza migogoro inayoweza kujitokeza katika mazingira ya kazi.

Vilevile, nyimbo za uvuvi hutumika kuhifadhi na kueneza maarifa ya jadi yanayohusiana na shughuli za uvuvi. Kupitia nyimbo hizo, vijana hujifunza mbinu za uvuvi, maadili ya kazi, tahadhari za usalama na uzoefu wa wazee wao kuhusu mazingira ya Ziwa Victoria. Hivyo, nyimbo huwa daraja muhimu la kurithisha maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuhakikisha kuwa utamaduni wa jamii unaendelea kudumishwa.

Kwa upande mwingine, nyimbo hizi hutumika kama njia ya kueleza hisia, mitazamo na uzoefu wa maisha ya wavuvi. Kupitia nyimbo, wavuvi huweza kueleza furaha wanapopata mavuno mazuri ya samaki, huzuni wanapokumbwa na misiba au hasara, pamoja na matarajio yao kuhusu maisha na kazi zao. Kwa kufanya hivyo, nyimbo zinakuwa njia muhimu ya mawasiliano inayoweza wanajamii kushiriki hisia na uzoefu wao kwa pamoja.

Kwa ujumla, matumizi ya nyimbo za uvuvi za Kisukuma kama nyenzo za mawasiliano yanatokana na uwezo wake wa kuwasilisha taarifa, kuhamasisha uwajibikaji, kuimarisha mshikamano wa kijamii, kuhifadhi maarifa ya jadi na kueleza hisia za wanajamii. Kutokana na umuhimu huo, nyimbo hizi zimeendelea kuwa sehemu muhimu ya maisha ya wavuvi na chombo madhubuti cha mawasiliano katika jamii ya Wasukuma wa

mwambao wa Ziwa Victoria.

MAPITIO YA MACHAPISHO MBALIMBALI

Mapitio ya machapisho ni sehemu muhimu ya utafiti inayomwezesha mtafiti kutambua mawazo, nadharia na matokeo ya tafiti zilizotangulia kuhusu mada husika. Katika makala hii, mapitio ya maandiko yanajikita katika dhana za nyimbo, uvuvi na mawasiliano kwa kuwa ndizo nguzo kuu zinazounda msingi wa uchunguzi huu kuhusu nyimbo za uvuvi za Kisukuma kama nyenzo ya mawasiliano ya jamii.

Nyimbo ni mojawapo ya vipengele muhimu vya fasihi simulizi vinavyotumika kuwasilisha mawazo, hisia, maarifa na uzoefu wa jamii husika. Katika jamii mbalimbali duniani, nyimbo zimekuwa sehemu muhimu ya maisha ya watu na hutumika katika shughuli za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Aidha, nyimbo ni miongoni mwa kazi za sanaa zinazobeba ujumbe wenye maana kwa jamii. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), sanaa ni ufundi wa hali ya juu wa kuwasilisha mawazo, hisia na uzoefu kwa namna inayoweza kuathiri hisia na fikra za hadhira. Kwa msingi huo, nyimbo za uvuvi za Kisukuma zinaweza kutazamwa kama kazi za sanaa zinazobeba ujumbe muhimu wa kijamii na kiuchumi miongoni mwa wavuvi wa mwambao wa Ziwa Victoria.

Nyimbo kama Kipengele cha Fasihi

Wataalamu mbalimbali wamejadili dhana ya nyimbo kwa mitazamo tofauti. Omary na Mvungi (1981) wanaeleza kuwa nyimbo ni sehemu ya fasihi simulizi ya kimapokeo inayorithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine. Kwa mujibu wao, nyimbo ni urithi wa jamii unaobeba uzoefu, maadili na maarifa yanayohifadhiwa kupitia mchakato wa urithishaji wa kitamaduni.

Mulokozi (1996) anafasili nyimbo kuwa ni utanzu wa ushairi katika fasihi simulizi unaoimbwa na kuambatana na muziki wa sauti. Anaongeza kuwa nyimbo hutumika kuwasilisha ujumbe mbalimbali unaohusu maisha ya jamii. Naye Nketia (1963) anaeleza kuwa nyimbo huakisi shughuli za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kidini zinazofanyika katika jamii husika. Kwa mtazamo wake, nyimbo ni njia mojawapo ya kueleza hisia na mitazamo ya wanajamii kuhusu matukio mbalimbali ya maisha.

Aidha, Mulokozi (1996) anasisitiza kuwa nyimbo zina dhima nyingi katika jamii, ikiwemo kuburudisha, kuelimisha, kuonya, kuhamasisha na kuadilisha tabia za wanajamii. Kutokana na dhima hizo, nyimbo zimeendelea kuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano inayoweza jamii kushirikiana, kujifunza na kuhifadhi utamaduni wake. Hivyo, nyimbo za uvuvi za Kisukuma

zinaweza kutazamwa kama sehemu ya fasihi simulizi inayotumika kuwasilisha ujumbe na kuratibu shughuli za uvuvi miongoni mwa wavuvi.

Dhana ya Uvuvi

Uvuvi ni mojawapo ya shughuli muhimu za kiuchumi zinazofanywa katika maeneo yenye rasilimali za maji kama vile maziwa, mito na bahari. Anderson (1986) anaeleza kuwa uvuvi ni mfumo wa uzalishaji unaotegemea matumizi ya rasilimali za asili zinazopatikana katika mazingira ya majini kwa ajili ya kupata chakula na kipato. Kwa upande mwingine, United Nations Economic and Social Commission for Western Asia (UNESCWA) inaifasili dhana ya uvuvi kuwa ni shughuli ya kuvuna viumbe wa majini kutoka katika mazingira ya asili au yaliyoboreshwa kwa matumizi ya binadamu. Nayo Intergovernmental Platform on Biodiversity and Ecosystem Services (IPBES) inaona uvuvi kama shughuli inayohusisha uvunaji wa viumbe wa majini kwa kuzingatia misingi ya kisayansi, kijamii na kiuchumi ili kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

Katika mazingira ya uvuvi, nyimbo zimekuwa sehemu muhimu ya maisha ya wavuvi. Nyimbo za uvuvi huimbwa wakati wa safari za majini au wakati wa utekelezaji wa shughuli za uvuvi. Kwa mujibu wa Kelvin (2017), nyimbo hizi hubeba maudhui mbalimbali kama vile kuhamasisha ari ya kazi, kuomba mafanikio, kueleza uzoefu wa maisha ya wavuvi na kuimarisha mshikamano wa kijamii. Hivyo, nyimbo za uvuvi ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii zinazojishughulisha na shughuli za uvuvi.

Dhana ya Mawasiliano

Mawasiliano ni mchakato muhimu unaoweza kubadilishana taarifa, mawazo, hisia na ujumbe kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kujenga uelewano. DeVito (2009) anafasili mawasiliano kuwa ni mchakato wa kutuma na kupokea ujumbe kwa kutumia alama au ishara zenye maana. Shannon na Weaver (1949) wanaeleza mawasiliano kama mchakato wa kupitisha ujumbe kutoka kwa mtumaji kwenda kwa mpokeaji kupitia njia maalumu huku ukikabiliwa na changamoto mbalimbali zinazoweza kuathiri ufanisi wake.

Naye Schramm (1954) anabainisha kuwa mawasiliano ni mchakato wa kushirikishana taarifa kwa kutumia alama au misimbo inayofahamika kwa wahusika wote wanaohusika katika mawasiliano. Kwa ujumla, mawasiliano ni mchakato wa kubadilishana taarifa, mawazo, hisia na uzoefu kwa kutumia njia mbalimbali kama vile lugha ya mazungumzo, maandishi, ishara, vitendo na nyimbo.

Massamba (2009) anafafanua mawasiliano kuwa ni upashanaji wa habari kwa kutumia misimbo inayotambulika kwa pande zinazohusika. Nayo TUKI (2012) inaeleza kuwa mawasiliano ni upashanaji wa habari kwa njia mbalimbali zinazoweza ujumbe kufikishwa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine. Mitazamo hii inaonesha kuwa mawasiliano yanaweza kufanyika kupitia njia tofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya jamii husika.

Katika muktadha wa fasihi simulizi, nyimbo ni mojawapo ya njia muhimu za mawasiliano. Balisidya (1989) anaeleza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zinazojengwa kwa kutumia mahadhi, melodia, mapigo na urari wa sauti ili kuwasilisha ujumbe fulani. Aidha, Mgeni (2014) anabainisha kuwa nyimbo ni utanzu muhimu wa fasihi simulizi uliotumika kwa muda mrefu katika jamii mbalimbali duniani kama njia ya kuhifadhi na kuwasilisha maarifa.

Kwa mujibu wa Sengo (1978) na Finnegan (1977), chimbuko la nyimbo linahusishwa na shughuli za uzalishaji mali ambazo binadamu walizifanya katika mapambano yao dhidi ya mazingira. Naye Senkoro (1989) anaeleza kuwa nyimbo zilianza kama sehemu ya kazi na zilitumika kupunguza uchovu, kuongeza ari ya kazi na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa washiriki wa shughuli mbalimbali za uzalishaji. Mtazamo huu unaendana na matumizi ya nyimbo za uvuvi za Kisukuma ambazo huimbwa na wavuvi ili kuhamasisha uwajibikaji, kuimarisha mshikamano na kuwezesha mawasiliano wakati wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Victoria.

NADHARIA YA UTAFITI

Makala hii imeongozwa na nadharia ya uamilifu katika kubaini mambo ambayo binadamu hushiriki katika mazingira yake ili kuweza kukidhi malengo yao kiuchumi haswa katika shughuli za uvuvi kwa kutumia nyimbo kama nyenzo za mawasiliano. TUKI (2004:300) wanasema “nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Pia kwa mujibu wa Wamitila (2003:22) anasema kwamba, nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kuelezea hali fulani, chanzo chake, muundo wake, utenda kazi wake na mwingiliano wa ndani na nje.

Naye Wafula na Njogu (2007:7) wamefasili dhana ya nadharia kama ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi hii imeegemea hasa katika nadharia ya uhakiki wa fasihi. Pia imetaja vitu muhimu kama vile, maelekezo ambayo

ndiyo yanamuongoza msomaji au mhakiki ili asivuke mipaka ya mawazo ya hiyo nadharia atumiayo ili kufanikisha kazi kwa ufasaha. Kwa mujibu wa Wamitila (2006) waasisi wa nadharia hii ya uamilifu ni pamoja na Bronislaw Malinowski, Raddiffe Brown na Franz Boazi. Nadharia ya uamilifu ni moja wapo ya nadharia zinazotumiwa kueleza namna ambayo binadamu wanavyoweza kushiriki ili kufikisha malengo yao ya pamoja katika mazingira tofauti. Nadharia hii inalenga hasa katika kuelezea hatua za uamilifu katika mazingira ya kiraia, kisiasa na kiuchumi. Nadharia hii inaeleza kuwa jamii inaweza kuchukuliwa kama mfumo ulio na sehemu zenye uamilifu yaani sehemu zinazotenda kazi, Boundless (2016). Nadharia hii inaeleza kuwa kila jamii ni huru na huchangia katika ufanyakazi wa jamii, hivyo ikiwa jamii haitaweza kuchangia katika ufanyakazi wa jamii basi jamii hiyo haitafanikiwa. Hapa kuna mihimili kadhaa ya uamilifu.

Hirschman, A. O, (1970), katika andiko lake Hirschman anaelezea jinsi watu wanavyojibu hali mbaya ya kupitiwa na uamuzi wa kuondoka (exist) au kushiriki (voice) katika mchakato wa mabadiliko, akisisitiza umuhimu wa ushirikiano. Putnam, R.D, (2000), anaangazia jinsi ushirikiano wa mtandao wa kijamii unavyoathiri maendeleo ya jamii akionyesha umuhimu wa ushirikiano kujenga uhusiano mzuri wa kijamii. Fukuysla, F, (1995), Anajadili jinsi imani na ushirikiano kati ya watu vinavyoweza kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Coleman, J. S, (1988), anasisitiza umuhimu wa mtaji wa kijamii katika ujenzi wa uwezo wa kibinadamu na jinsi ushirikiano unavyoweza kuimarisha jamii.

Giddes, A, (1990), anaeleza mabadiliko ya kijamii na kisiasa akishughulikia jinsi ushirikiano katika jamii unavyoweza kuathiri maendeleo na uhusiano wa kibinadamu. Emery, F. E& Trist, E. L, (1965), wanaandika kuhusu jinsi mazingira yanavyoweza kuathiri ushirikiano ndani ya mashirika na umuhimu wa muktadha katika kutaja maana. Msingi wa ushirikiano, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya watu binafsi na makundi. Uamilifu unahusisha kutoa na kupokea msaada kutoka kwa wengine ili kufikia malengo ya pamoja.

Mabadiliko ya kijamii, uamilifu unatoa nafasi ya kujadili na kurekebisha hali za jamii na kisiasa zinazoweza kuathiri watu. Hii inahusisha kufanya kazi pamoja ili kuboresha mazingira ya jamii. Mabadiliko ya uamuzi, katika muktadha wa uamilifu, uamuzi sio jambo la mtu mmoja tu bali linaweza kuwa na ushawishi wa makundi mbalimbali. Uamilifu unategemea ushirikiano wa

pamoja ili kufanya maamuzi bora. Rasilimali na uwezo, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa kutumia rasilimali zilizopo kwa kushirikiana ili kufikisha malengo yaliyokusudiwa.

Ushirikiano wa kimaendeleo, uamilifu unahusisha ushirikiano katika mipango ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hii inajumuisha kushirikiana katika mipango ya maendeleo endelevu na kuunda nafasi za ajira. Ukuaji kijamii kwa kushirikiana, jamii zinaweza kukua kimaendeleo kwa kiasi kikubwa ambapo wanajamii wanajifunza kutoka kwa wenzao na kuimarisha mtandao wa msaada. Hivyo ndivyo mihimili ya nadharia ya uamilifu inavyoweza kuwasilishwa na inaleta mwangaza juu ya umuhimu wa ushirikiano katika maendeleo ya jamii na uhusiano wa kibinadamu. Nadharia ya uamilifu imeasisiwa au imeanzishwa na waasisi tofauti tofauti ambao ni Hirschman, A. O, (1970), Fukuyama F, (1995) na Coleman, J.S (1988). Suala la ushuhudia ni kuona tukio fulani wewe mwenyewe bila kuambiwa na mtu mwingine. Enon (1995) anaeleza kuwa ushuhudiaji unamfanya mtafiti aweze kushiriki katika tukio na kuona ukweli katika kupata data. Watafiti walishiriki kuona na kusikiliza jinsi wavuvi wanavyoimba nyimbo zao na kuweza kuwasiliana. Usaili ni mazungumzo yanayoambatana na maswali anayoulizwa mtu na mtu mwingine ili kudadisi taarifa fulani. Mtafiti ndiye huwa mhojaji na mtafiti ndiye mtoa majibu, njia hii ni ya mahojiano ya mwingiliano wa papo kwa papo (Walter, 1989). Hivyo ulitumia njia ya maelezo (Creswell, 1988) anaeleza muundo wa utafiti kama ni mtazamo wa kifika ambao unamwongoza mtafiti katika utafiti. Kothari (2004) anasema mkabala huu unamwezesha mtafiti kufafanua maoni na maelezo yanayotolewa ni mkabala unaozingatia upataji wa data katika uhalisia wake na tafsiri inayotolewa na watafiti (Creswell, 1998, Alvesson na Sholdeberg, 2009). Hivyo watafiti walipata fursa ya kupata muda wa kuhojiana na watafitiwa ana kwa ana ambapo njia hii iliwapata nafasi watafiti kufanya mahojiano ya kina zaidi ambayo huhitaji ujuzi na ukamilifu katika kumwongoza mhojiwa kutoa taarifa zinazohitajika.

MBINU ZA UTAFITI

Mbinu za utafiti ni taratibu na mikakati inayotumiwa na mtafiti katika kukusanya, kuchambua na kutafsiri data ili kujibu maswali ya utafiti au kufikia malengo yaliyowekwa. Kwa mujibu wa C.R. Kothari (2004), mbinu za utafiti ni njia za kisayansi zinazomwezesha mtafiti kupata taarifa sahihi na za kuaminika kuhusu

jambo linalochunguzwa. Naye John W. Creswell (2014) anaeleza kuwa mbinu za utafiti ni mchakato unaojumuisha ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa data kwa kutumia mikabala na taratibu zinazokubalika kitaaluma.

Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaeezo (*qualitative approach*) kwa kuwa ulihusisha uchunguzi wa nyimbo za uvuvi za Kisukuma na namna zinavyotumika kama nyenzo ya mawasiliano ya jamii. Mkabala huu ulimwezesha mtafiti kupata taarifa za kina kuhusu uzoefu, mtazamo na matumizi ya nyimbo hizo katika mazingira halisi ya shughuli za uvuvi.

Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanyika katika Kata ya Luchelele, Mtaa wa Sweya, Wilaya ya Nyamagana, Mkoa wa Mwanza. Eneo hili lilichaguliwa kwa sababu ni mojawapo ya maeneo ya mwambao wa Ziwa Victoria yenye shughuli nyingi za uvuvi na jamii kubwa ya wavuvi wa Kisukuma. Hivyo, eneo hilo lilitoa mazingira mwafaka ya kupata data zinazohusiana na nyimbo za uvuvi na matumizi yake katika mawasiliano ya kijamii.

Washiriki wa Utafiti

Washiriki wa utafiti huu walikuwa wavuvi wa jamii ya Wasukuma wanaojishughulisha na shughuli za uvuvi katika mwambao wa Ziwa Victoria. Washiriki hao walichaguliwa kwa kuwa wana uzoefu wa moja kwa moja kuhusu matumizi ya nyimbo za uvuvi katika shughuli zao za kila siku.

Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usaili na ushuhudiaji shirikishi. Mbinu ya usaili ilitumika kupata taarifa kuhusu matumizi, maudhui na dhima za nyimbo za uvuvi miongoni mwa wavuvi. Aidha, ushuhudiaji shirikishi ulimwezesha mtafiti kushuhudia na kurekodi namna nyimbo hizo zinavyoimbwa na kutumika katika mazingira halisi ya uvuvi.

Mbinu za Uchambuzi wa Data

Data zilizokusanywa zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa uchambuzi wa kimaudhui. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kubainisha dhamira, ujumbe na dhima mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo za uvuvi za Kisukuma, hususan katika kuimarisha mawasiliano, mshikamano wa kijamii na uwajibikaji miongoni mwa wavuvi.

Masuala ya Maadili ya Utafiti

Katika utekelezaji wa utafiti huu, kanuni za maadili ya utafiti zilizingatiwa. Washiriki walipewa maelezo kuhusu madhumuni ya utafiti na walishiriki kwa hiari. Aidha, taarifa walizotoa zilitunzwa kwa usiri na zilitumika kwa

madhumuni ya kitaaluma pekee.

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

Sehemu hii imelenga kuwasilisha na kutoa ufafanuzi wa kina wa uchambuzi wa data zilizopatikana katika utafiti huu. Data za utafiti zimechambuliwa kwa kuzingatia lengo kuu la kuchunguza mchango wa nyimbo za uvuvi za kisukuma kama nyenzo za kuimarisha mawasiliano. Nyimbo za kisukuma za uvuvi ni nyimbo ambazo huimbwa na wavuvi wakiwa katika shughuli hiyo. Nyimbo hizo huwa zinambwa kwa malengo tofautitofauti ambapo kupitia kuimba hizo nyimbo ndipo mawasiliano hufanyika kwani wavuvi huwasiliana na kuelewana kupitia hizo nyimbo zao wakati wa uvuvi. Miongoni mwa majukumu ya nyimbo hizo ni pamoja na;

Kuhamasisha Uwajibikaji

Nyimbo za uvuvi zinapoimbwa huwatia nguvu wavuvi wakati wa shughuli hiyo ambayo imeonekana kuwa ngumu na yenye hatari kubwa. Kupitia nyimbo ambazo wanaziimba wavuvi wakiwa katika shughuli za uvuvi zimeonekana kusaidia kuwaondolea woga kwa kuwatia nguvu katika uwajibikaji bila kuchoka. Katika kushadadia suala hili, kuna nyimbo mbalimbali za kisukuma ambazo wavuvi huimba wakati wakiwa wanavua ili kutiana hamasa na nyimbo hizo zinatunika katika upashanaji wa habari au taarifa kati ya wavuvi na wavuvi wengine, hii ni kutokana na baadhi ya wavuvi kuonekana kutegea kazi hivyo huo wimbo ukiimbwa wale wavuvi waliokuwa hawafanyi kazi vizuri huelewa na kuonyesha mwitiko wa kufanya kazi kwa bidii, ufuatao wimbo unaodhihirisha hayo;

Mpaga kwishunguli olutali mdunia
Nu bhabha Murungu nanhwe akukwambilija
Waliwaluhano uluka ng'wana lemi
Mulibhona ihaha mashine ikopogomaga
Nukukaya bhoya nakuzwelwa

Tafsiri yake kwa Kiswahili

Lazima kujishungulisha ukiwa bado duniani
Na Mungu naye atasiadia
Alikuwa ameteseka mno Luka mtoto wa Lemi
Mnaona sasa hivi mashine inaunguruma
Na nyumbani kwao paa halivuji.

Hivyo ukirejelea katika mstari wa kwanza (1) ni dhahiri kuwa ni lazima kufanya kazi kwa bidi ili kuepuka umaskini, wimbo huu unapoimbwa husaidia kuwasiliana baina ya wavuvi na kuwatia hamasa na nguvu ya kufanya kazi kwa bidii, kupitia maneno ya wimbo huu wavuvi hupata nguvu na moyo wa kuendelea kuvua samaki kwa bidi ili wapate Samaki kwa ajili ya kujiinua kiuchumi. Vivyovivyo katika mstari

wanne (4) anaposema “Na nyumbani kwao paa halivuji” kauli hii inawatia nguvu ili siku moja wawe na maisha mazuri na kusaidia wazazi wao pia.

Oduka nyanza ondukila unchoji
Oliobhubhi ukanje nani
Bhakwiza kuhisha bhujiku welagha
Bhise yaya kushoka numa tulemice

Tafsiri yake kwa Kiswahili

Unatukana ziwa unamtukana mtafutaji
Wewe uko mbaya umtishie nani
Watashituka usingizini usiku umeshaisha
Sisi hapana kurudi nyuma tume shakataa

Wimbo huu unapoibwa husaidia mawasiliano baina ya wavuvi kwani kupitia huu wimbo mawasiliano baina ya wavuvi kupitia maneno ya wimbo huu husaidia kuwasiliana kati ya mvuvi mmoja na mwingine na kusaidia kutiana hamasa na nguvu ya kufanya kazi kwa bidii. Mawasiliano haya yapapofanyika kwa ufasaha na kueleweka kwa wavuvi hao, husaidia wavuvi kufanya kazi kujituma zaidi.

Kuhamasisha Hisia na Mwelekeo katika Kazi

Nyimbo huwa na nguvu ya kuhamasisha hisia kwa wavuvi pindi wanapofanya kazi katika mazingira magumu ya uvuvi, hivyo kuna nyimbo zinazoonyesha hisia za huzuni, furaha na katika nyimbo za uvuvi za kisukuma.

a) Nyimbo za Uvuvi za Kisukuma zenye Kudhihirisha Hisia za Huzuni

Wavuvi wakiwa katika shughuli zao huimba nyimbo ambazo hudhihirisha huzuni baina yao. Nyimbo hizo zinapokuwa zikiimbwa wavuvi hao hujua kabisa kwamba kuna jambo la huzuni kati yao hivyo kutumika kama sehemu ya kutoa mawasiliano miongoni mwao. Hali kama hii uwepo wa tukio la huzuni miongoni mwa wavuvi na wengine baada ya kupata taarifa kupitia nyimbo hizo huweza kupata huzuni na uchungu kiasi cha kuanza kulia. Huzuni hiyo huweza kutokana na mambo kama vile mvuvi mwenzao kukamatwa na Afisa uvuvi au kukumbuka mwenzao ambaye alishawahi kupoteza maisha siku za nyuma. Ukweli huu unadhihirika kupitia wimbo ufuatao;

Wan'gwakawili mayo nalikhunu
Zughu nalabukaga natinangunani
Sama ndito tulifuma Msalala
Twenganga Nyantungu tugobelwa mnzila
Badumha kulima tukiza kubasanga
Tutalitulila twizukwa maombolezo
Ong'wabhebhe Rais ukambarage Nyerere
Watulekela huzuni Batanzania
Nulutulile mwisho tutachoka

Yamala kukundikija lwelelo.

Tafsiri yake katika Kiswahili

Mtoto wa kawili mama nipo huko
Njoo nimeumia Sina msaada
Kuhama kugumu tunatoka msalala
Tumetoka Nyantunguja tukatekwa njiani
Wasiojua kulima tuliwakuta
Bado tunalia tunakumbuka maombolezo
Ya baba Rais Kambarage Nyerere
Umetuachia huzuni watanzania
Hata tukilia mwishi tutachoka
Dunia ilishafunika

Hivyo ukirejelea katika mstari wa tisa (9) na kumi (10) mwimbaji katika wimbo hapo juu, mwimbaji anaonesha kuwa wanaomboleza kuhusu Rais wa kwanza wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alikua anawatetea wavuvi wadogowadogo. Hivyo basi wimbo huu unapoimbwa wavuvi huwasiliana baina yao kwani huwasaidia wao kwa wao kutambua kuwa kuna jambo la huzuni baina yao.

b) Nyimbo za Wavuvi za Kisukuma Zinazohamasisha Furaha

Wakati wa uvuvi nyimbo huimbwa ili kuwapa wavuvi furaha kwa hushangilia mafanikio ya kazi yao kwa kupata mathalani samaki wengi. Hivyo mvuvi anaposikia wimbo huu anapata taarifa kuhusu mafanikio yaliyopatikana na kuweza kuungana na wavuvi wengine kufurahia. Furaha hii inarejelewa katika wimbo ufuatao;

Wang'waga walya umasomhe
Walyaga chengu kunona
Walyaga Wiluma na nzwala
Jasa ulibhuja ng'wabudaga
Galicho mashimbe mamageni
Gababele sawa na mwicha

Tafsiri yake katika Kiswahili

Alikuwa anakunywea pombe Masomhe
Alikuwa anakula sangara watamu
Alikuwa anakula anajing'ata na vidole
Nenda unauliza kwa Bhudaga
Wapo wasimbe akina mageni
Wanamatiti kama matunda

Katika wimbo tajwa hapo juu unahamasisha wavuvi kufurahia mafanikio ya uvuvi wao. Hivyo mawasiliano yanatokea pale mvuvi anaposikia wimbo huu unaimbwa na kushiriki vyema katika furaha hiyo. Pia hata wale wanaokuwa karibu na wavuvi hao hutambua mafanikio ya kupata samaki wengi kwa wavuvi hao. Kupitia wimbo huu hutoa mchango mkubwa kama nyenzo ya mawasiliano baina ya watu na wavuvi katika shughuli

zao.

Nyimbo za Uvuvi za Kisukuma Hudhihirisha hali ya Hatari

Katika shughuli ya uvivu kuna changamoto mbalimbali ambazo wakati mwingine huwa zinakwamisha zoezi la uvuvi. Hivyo katika njia ya kuepuka madhara au hatari inayoweza kupatikana, wavuvi huimba wimbo ambao hutoa taarifa kuwa wavuvi wengine, huimba wimbo ambao hutoa taarifa kuwa wavuvi wengine au watu waliopo ziwani kusitisha shughuli zao kwa muda ili kuepuka hatari hiyo iliyo mbele yao. Hivyo kupitia wimbo huo taarifa huwafikia wavuvi na mawasiliano hutekelezeka kwa muda huo. Mawasiliano hayo hudhihirika mfano katika wimbo ufutao;

Liyaga lyafuma litungile mkiya
Nchoji shokaga ukujugulala
Bhanhu bhinge bhaka chage

Tafsiri yake katika Kiswahili

Upepo umetoka unaelekea mashariki
Mtafutaji rudi utaenda ukafariki
Watu wengi wamekufa

Kwa kurejelea mstari wa kwanza katika wimbo huo unatoa taarifa ya hatari ya kuwepo kwa upepo ambao hukwamisha suala la wavuvi kuendelea na shughuli za uvuvi, hivyo wavuvi wanaposikia wimbo huu hupata taarifa ya kuwepo kwa hatari ziwani. Hivyo wasitisha kazi na wanaojiandaa kwenda wasubiri kwa sababu hali mbaya ya upepo ziwani huweza kusababisha vifo kwa wavuvi. Mawasiliano hapa yanatokea na kufanikiwa kwa asilimia kubwa huku wavuvi wanaopokea taarifa iliyotolewa na kusitisha kazi ya uvuvi ili kuepuka hatari hiyo. Hatari hiyo huhusisha uwepo wa mawimbi makubwa ambapo wavuvi wanaposikia wimbo huweza kutua nanga na kurudi mwaroni ili kusubiri mawimbi yaishe na ziwa litulie ili kuendelea na kazi ya kuvua samaki. Wimbo huu wa uvuvi una mchango mkubwa katika kufanikisha mawasiliano ya wavuvi katika shughuli zao.

MAPENDEKEZO

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, inapendekezwa kuwa serikali, taasisi za utamaduni na wadau mbalimbali wa maendeleo wachukue hatua za makusudi za kuhifadhi na kuendeleza nyimbo za uvuvi za Kisukuma kwa kuwa ni sehemu muhimu ya urithi wa utamaduni na nyenzo madhubuti ya mawasiliano ya jamii. Juhudi hizo zinaweza kujumuisha kurekodi nyimbo hizi, kuzihifadhi katika nyaraka za kitaifa na kuzitambulisha kwa vizazi vipya kupitia shughuli mbalimbali za kitamaduni na kielimu.

Aidha, taasisi za elimu zinashauriwa kuzingatia fasihi simulizi za jamii mbalimbali, ikiwemo nyimbo za uvuvi za Kisukuma, katika ufundishaji wa lugha na utamaduni. Hatua hii itasaidia wanafunzi kuelewa umuhimu wa nyimbo hizi katika kuwasilisha maarifa, maadili na uzoefu wa maisha ya jamii husika. Vilevile, watafiti wanahimizwa kufanya tafiti zaidi kuhusu nyimbo za uvuvi na aina nyingine za fasihi simulizi ili kubaini mchango wake katika nyanja mbalimbali za maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Kwa upande mwingine, mashirika yanayohusika na maendeleo ya sekta ya uvuvi yanapaswa kutumia nyimbo za jadi kama nyenzo ya kuelimisha jamii kuhusu usalama ziwani, uhifadhi wa mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali za maji. Kwa kuwa nyimbo hizi zinaeleweka kwa urahisi na kukubalika miongoni mwa wanajamii, zinaweza kutumika kufikisha ujumbe muhimu kwa ufanisi zaidi. Vilevile, viongozi wa jamii wanapaswa kuhamasisha matumizi ya nyimbo hizi katika kuendeleza mshikamano, uwajibikaji na maadili ya kazi miongoni mwa wavuvi na wanajamii kwa ujumla. Kwa ujumla, kuna haja ya kutambua nyimbo za uvuvi za Kisukuma si kama chombo cha burudani pekee, bali kama nyenzo muhimu ya mawasiliano, elimu ya jadi na maendeleo ya jamii, ambayo inapaswa kuhifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

HITIMISHO

Makala hii imechunguza mchango wa nyimbo za uvuvi za Kisukuma kama chombo cha mawasiliano ya jamii miongoni mwa wavuvi wa mwambao wa Ziwa Viktoria. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa nyimbo hizi zina nafasi kubwa katika kuwasilisha taarifa, kuhamasisha uwajibikaji, kujenga mshikamano, kueleza hisia mbalimbali na kutoa tahadhari kuhusu hatari zinazoweza kujitokeza wakati wa shughuli za uvuvi. Kupitia nyimbo hizo, wavuvi huwasiliana kwa ufanisi, hujengeana moyo wa kufanya kazi kwa bidii na huimarisha ushirikiano katika kutekeleza shughuli zao za kiuchumi.

Aidha, utafiti umeonesha kuwa nyimbo za uvuvi za Kisukuma si nyenzo za burudani pekee, bali ni sehemu muhimu ya fasihi simulizi inayobeba maarifa, maadili, historia na uzoefu wa jamii ya Wasukuma. Kwa kuzingatia Nadharia ya Uamilifu, imeonekana kuwa nyimbo hizi hutekeleza majukumu muhimu ya kijamii kwa kuchangia ustawi wa jamii na kufanikisha shughuli za uzalishaji mali. Hivyo, kuna umuhimu wa kuzitambua, kuzithamini na kuzihifadhi nyimbo hizi

kama urithi hai wa utamaduni wa Kisukuma na kama chombo madhubuti cha mawasiliano kinachochangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika jamii husika.

MAREJELEO

- Anderso, L.G. (1986). *The Economics of Fisheries Management*. Johns Hopkins University Press.
- Balisidyo, M.L. (1989). *Uchunguzi katika Fasihi Simulizi Vizingiti na Makala* (Makala za Simulizi). Dar es Salaam: TUKI.
- Coleman, J.S. (1988). *Social Capital in the Creation of Human capital*. American Journal of Sociology, 94, 595-5120.
- Devita, J.A. (2009). *The Interpersonal Communication*. Book 12th Edition Person Education.
- Enon, J.C. (1995). *Education Research, Statistics and Measurement*. Kampala: Makerere University Press.
- Finnegan, R. (1970). *Oral poetry its nature, Significance and Social Context*. New York. Melbourne: Cambridge University Press.
- Fukuyama, F. (1995). *Trust: The Social Virtues and the Creation of Prosperity*. Free Press.
- Giddens, A. (1990). *The Consequences of Modernity*. Stanford University Press.
- Hirschman, A.O. (1970). *Exist Voice and Loyalty, Responses Decline in Forms, Organization and States*. Harvard University Press.
- Massamba, D.P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mazrui, A.M. & Syambo, B.K. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Educational Publishers.
- Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi Simulizi na Utamaduni wa Kiafrika*. Dar es Salaam: DP.
- Ndagala, D.K. (1980). *Traditional Leadership and Social Integration among the Sukuma*.
- Nketia, J.H. (1963). *Drumming in Akan Communities*. London: Thomas Nelson and Sons Ltd.
- Putnam, R.D. (2000). *Bowling Alone: The Collapse and Revival of American Community* Simon and Schuster.
- Sengo, T.S. (1978). *Towards Maturate in Kiswahili*. Kiswahili 54/1 a54/2.
- Senkoro, F.E.M.K. (1989). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.
- Shannon, C.E & Weaves, W. (1949). *The Mathematical Theory of Communication*. University of Illinois Press.
- TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es

Salaam: TUKI.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasili Simulizi na Andishi*. Nairobi: Kenya Focus Publications Ltd.

Wamitila, K.W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake*. Mombasa: Phoenix Publishers Ltd.